TANGAZO LA SERIKALI Na. 143 la tarehe 28/2/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

---

# SHERIA NDOGO

---

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA STENDI YA MABASI YA HALMASHAURI YA MJI NJOMBE YA MWAKA 2025

Jina

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Stendi ya Mabasi ya Halmashauri ya Mji Njombe ya Mwaka 2025.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Mji Njombe.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirishia bidhaa, abiria au mizigo isipokuwa wanyama;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji Njombe;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mmiliki'' maana yake ni mmiliki, kondakta au dereva anayetumia chombo cha usafiri katika eneo la kituo cha mabasi;

"stendi" au "kituo cha mabasi" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo,

na inajumuisha kituo cha kupaki malori na vituo vingine vidogo vya kupakia na kushusha abiria vya Halmashauri;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ada na ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii; na

"yadi" maana yake ni eneo lililotengwa kwa ajili ya kuhifadhi vyombo vya usafiri.

Ushuru wa stendi

**4**.-(1) Halmashauri itatoza ushuru kwa vyombo vyote vya usafiri vinavyoingia na kutoka ndani ya stendi kwa saa ishirini na nne kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Halmashauri itatoza ushuru kwa mtu anayeingia na kutoka stendi.

(3) Wakala au afisa yeyote wa Halmashauri atakayepokea malipo ya ushuru atatoa stakabadhi ya kielektroniki kulingana na malipo yaliyofanyika na tarehe ya tukio.

(4) Kila chombo cha usafiri kinachoingia katika eneo la stendi kinatakiwa kulipiwa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, malipo hayo yatafanyika kwa siku, mwezi au kwa kadri Halmashauri itakavyoona inafaa.

(5) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) na (2), magari ya kubeba wagonjwa na vyombo vya usafiri vinavyomilikiliwa na Serikali, wanadiplomasia au majeshi na havitatozwa ushuru.

Uanzishaji wa Kituo cha mabasi

**5**.-(1) Halmashauri itaanzisha kituo cha mabasi mahsusi kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), kampuni, taasisi au mtu binafsi anaweza kuanzisha na kusimamia kituo cha mabasi anayomiliki kwa nia ya kupakia na kushusha abiria na mizigo baada ya kupata kibali maalum cha Halmashauri kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(3) Chombo cha usafiri kinachosafirisha abiria ndani na nje ya Halmashauri kinapaswa kuingia stendi ya Halmashauri na kulipiwa ushuru isipokuwa kwa mmiliki wa chombo cha usafiri aliyepata kibali chini ya kanuni ndogo ya 8(1) ambaye kwa makubaliano na Halmashauri atalipa ushuru wa stendi kwa Afisa Mwidhiniwa kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

(4) Kituo cha mabasi cha Halmashauri kinaweza kutumika kwa ajili ya kuegesha na kulaza vyombo vya usafiri baada ya kibali.

Matumizi ya stendi

**6**.-(1) Kila mtu yeyote anayefanya biashara ya kusafirisha abiria atakuwa na wajibu wa kupakia na kushusha abiria au mizigo yao katika eneo la stendi.

(2) Muda wa kutumia stendi utakuwa kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa nne kamili usiku, isipokuwa kama kuna kibali cha Halmashauri.

(3) Isipokuwa kwa magari yanayopita kutoka maeneo mengine ya nje ya Halmashauri, magari yote yanayofanya biashara ya usafirishaji ndani ya Halmashauri yataanzia safari zake stendi zilizoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii au sheria nyingine yoyote.

(4) Dereva wa gari ya abiria hataruhusiwa kusimamisha gari kwa zaidi ya dakika tano katika kituo cha njiani.

Wajibu wa kuingiza gari kituo cha mabasi

**7**.-(1) Itakuwa ni wajibu kwa kila dereva wa gari la abiria na mizigo litokalo ndani na kwenda nje ya Halmashauri na maeneo mengine ndani ya Halmashauri kuingiza gari katika eneo lililotengwa na Halmashuri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria na au mizigo.

(2) Magari yote ya abiria yatakuwa na maandishi yanayoonesha mahali yanapotoka na yanakoelekea.

(3) Dereva wa gari itakayoingia kituo cha mabasi atahakikisha gari inaingia kwa kutumia mlango wa kuingilia na kutoka kupitia katika mlango kutokea.

(4) Halmashauri itaweka utaratibu wa pikipiki kuingia na kutoka katika kituo cha mabasi.

Vituo vya mabasi binafsi

**8**.-(1) Halmashauri inaweza kutoa kibali cha kuanzisha kituo binafsi cha mabasi endapo itaona kuna umuhimu wa kuanzisha kituo hicho. kwa

(2) Kibali cha kuanzisha kituo binafsi kitakuwa kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kitatolewa baada ya mwombaji kuzingatia masharti yatakoyotolewa na Halmashauri na kulipia gharama kama zilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

(2) Halmashauri inaweza kusitisha wakati wowote kibali cha kuanzisha kituo binafsi kwa kutoa taarifa ya maandishi ya mwezi mmoja kwa mmiliki au mwendeshaji wa kituo.

Kulaza chombo cha usafiri ndani ya stendi

**9**.-(1) Halmashauri itaweka utaratibu wa kulaza vyombo vya usafiri ndani ya stendi.

(2) Halmashauri itatoza ushuru wa kulaza chombo cha usafiri ndani ya stendi.

Wajibu wa kutunza usafi

**10**. Kila mmiliki, dereva au kondakta wa chombo cha usafiri na kila msafiri au mtumiaji yeyote wa stendi au eneo lolote lililotengwa kwa ajili ya maegesho anatakiwa kuhakikisha kuwa hachafui au kusababisha uchafuzi wowote wa eneo la stendi au maegesho kwa kutupa taka, kumwaga au kusababisha kumwagika kwa maji au mafuta ya aina yoyote kwenye kituo cha mabasi.

Uteuzi wa Wakala

**11**.-(1) Halmashauri inaweza kuteua Wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kwa ajili ya kukusanya ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii; na

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Biashara ndogondogo

**12**. Mtu yeyote anayefanya biashara ndogo ndogo ataruhusiwa kufanya biashara ndani ya eneo la stendi bila masharti, isipokuwa anaweza kukubaliana na uongozi wa stendi kuhusu utaratibu wa ulinzi na usalama wake na mali zake.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

**13**.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kukamata na kuondoa chombo cha usafiri ambacho kitapakia au kushusha abiria nje ya eneo la stendi.

(2) Chombo cha usafiri kilichokamatwa kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (1) kitaondolewa na kuhifadhiwa kwenye yadi ya Halmashauri au sehemu yoyote kama itakavyoamriwa na Mkurugenzi.

(3) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuuza chombo kilichokamatwa baada ya kupata idhini ya mahakama endapo mmiliki wa chombo hicho atashindwa kulipa gharama za uangalizi pamoja na gharama za kukamata chombo hicho ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kukamatwa.

(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (3), kabla ya Halmashauri kuuza chombo kilichokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya maandishi kwa umma ya siku zisizozidi saba kuhusu kusudio la kuuza chombo hicho.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukamata au kushikilia chombo cha usafiri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala.

Kukamata na kuzuia chombo cha usafiri

**14.**-(1) Halmashauri inaweza kukamata na kuzuia chombo cha usafiri ambacho hakijalipiwa ushuru au ambacho mmiliki au dereva wake amekiuka sharti lolote katika Sheria Ndogo hii.

(2) Mmiliki au dereva wa chombo cha usafiri kilichokamatwa atapaswa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya muda wa siku mbili.

(3) Endapo ushuru hautalipwa baada ya muda wa siku mbili kupita tangu kukamatwa kwa chombo cha usafiri, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuuza chombo husika kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini

ya mahakama.

(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (3), kabla ya Halmashauri kuuza chombo kilichokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza chombo husika.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukamata au kuhifadhi chombo cha usafiri kilichokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri ikiwa ni pamoja na mali zilizo ndani ya chombo cha usafiri husika, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa kwa uzembe wa watumishi wa Halmashauri au Wakala.

Wajibu wa kuvaa sare na vitambulisho

**15**. Kila mfanyabiashara au wakala wa basi, muuza tiketi, mbeba mizigo, mfanyabiashara ndogondogo, mama lishe au baba lishe ndani ya stendi-

(a) anapaswa kuwa na kitambulisho maalumu kitakachotolewa na Halmashauri; na

(b) ana wajibu wa kuvaa sare maalumu wakati wote anapofanya shughuli zake katika eneo la stendi.

Makosa

**16**. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) atakataa, atashindwa au atamshawishi mtu yeyote kukataa kulipa ushuru;

(b) atapakia au kushusha abiria au mizigo katika eneo tofauti na stendi au eneo ambalo halikutengwa kwa ajili hiyo;

(c) atapiga debe katika eneo la stendi;

(d) atafanya matengenezo au kuosha gari katika eneo la stendi;

(e) atalaza chombo cha usafiri katika eneo la stendi bila kibali;

(f) atauza chakula au vinywaji au bidhaa nyingine bila kusajiliwa; au

(g) ataanzisha stendi au kituo cha mabasi kinyume na utaratibu ulioainishwa.

Adhabu

**17**. Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kutenda kosa chini ya Sheria Ngodo hii atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi

milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

**18.** Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii na kulipa ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo TS. Na. 124 la 2008

**19**. Sheria Ngodo hii inafuta Sheria Ndogo za (Stendi ya Mabasi) za Halmashauri ya Mji Njombe za Mwaka 2008.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

A: USHURU WA STENDI (KUINGIA NA KUTOKA)

| Na. | Aina ya Chombo cha usafiri | Kiwango cha ushuru (Shilingi) | Muda wa kutoza |
|---|---|---|---|
| 1. | Basi lenye uwezo wa kubeba abiria 5 hadi 15 | 2,000/= | Kila linapotoka |
| 2. | Basi lenye uwezo wa kubeba abiria 16 hadi 25 | 2,000/= | Kila linapotoka |
| 3. | Basi kubwa lenye uwezo wa kubeba abiria 26 hadi 35 | 2,000/= | Kila linapotoka |
| 4. | Basi kubwa lenye uwezo wa kubeba abiria 35 na zaidi | 3,000/= | Kila linapotoka |
| 5. | Teksi | 1,000/= | Kila linapotoka |
| 6. | Pikipiki ya magurudumu mawili | 3,00/= | Kila linapotoka |
| 7. | Pikipiki ya magurudumu matatu | 3,00/= | Kila linapotoka |
| 8. | Gari dogo aina ya Noah | 500/= | Kila linapotoka |
| 9. | Gari lolote dogo lisilotajwa hapo juu | 500/= | Kwa linapotoka |

B: USHURU WA STENDI (KULAZA CHOMBO CHA USAFIRI)

| Na. | Aina ya Chombo cha usafiri | Kiwango cha ushuru (Shilingi) kwa siku |
|---|---|---|
| 1. | Basi lenye uwezo wa kubeba abiria 5 hadi 15 | 3,000/= |
| 2. | Basi lenye uwezo wa kubeba abiria 16 hadi 25 | 3,000/= |
| 3. | Basi kubwa lenye uwezo wa kubeba abiria 26 hadi 35 | 3,000/= |
| 4. | Basi kubwa lenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 35 | 3,000/= |
| 5. | Teksi | 1,000/= |
| 6. | Pikipiki ya magurudumu mawili | 1,000/= |
| 7. | Pikipiki ya magurudumu matatu | 1,000/= |
| 8. | Gari dogo aina ya Noah | 1,500/= |
| 9. | Gari lolote dogo lisilotajwa hapo juu | 1,000/= |
| 10. | Magari ya mizigo | 5,000/= |

C: USHURU WA STENDI (MENGINEYO)

| Na. | Aina ya Ushuru | Kiwango cha ushuru (Shilingi) | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Mtu anayeingia au kutoka stendi | 200/= | kila anapoingia au kutoka |
| 2. | Wabeba mizigo stendi | 1,000/= | kwa siku |
| 3. | Wafanyabiashara biashara ndogo ndogo wasio na vitambulisho vya ujasiliamali | 1,000/= | kwa siku |
| 4. | Choo cha stendi | 300/= | kila anapoingia chooni |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 8 (1))*

FOMU YA KIBALI CHA KUANZISHA KITUO CHA MABASI BINAFSI

Kibali Na. ...................

Jina: ..................................................................................................
Anwani: ...........................................................................................
Namba ya NIDA: .............................................SIMU.........................
Namba ya Stakabadhi: .....................amelipa Sh..................................
Eneo Kituo kilipo: Mtaa:..……………Barabara:……..Jengo:………......…
Ukubwa wa eneo la Kituo au Maegesho (mita za mraba):…........
Kiasi kilicholipwa kwa miezi ………….. Jumla ya sh...............................
Muda wa kibali ni mwaka mmoja kuanzia ...................... hadi ......................
Maelezo mengine yatakayohitajika (kama yapo): ……………………………………………..………......………
………………………………………………………………………………………………………
………………

Kimetolewa tarehe…………mwezi……………….mwaka………..........…..

Kimetolewa na:
Jina: ………………………………………………………........……………..
Wadhifa:…………………………………………………….………………….
Saini................................................. Muhuri wa Ofisi:.…………....................
“*Fomu hii itawekwa katika Ofisi ya Kituo cha basi. Kumbuka kuzingatia Sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria Ndogo za Halmashauri*”.

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 18)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ...................................................................... nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ..................................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe, kwamba mnamo tarehe .......... ya mwezi .......................mwaka ........................... nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya...............ya Sheria Ndogo ya Stendi ya Mabasi ya Halmashauri ya Mji Njombe ya Mwaka 2025.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe, niko tayari kulipa ushuru ninaodaiwa wa kiasi cha shilingi …………………. pamoja na faini ya kufifilisha kosa ya kiasi cha shilingi ……………………….

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU NA KADRI YA UFAHAMU WANGU.
Leo tarehe .....................ya Mwezi ......................... Mwaka ......................................
Jina .................................................... Saini .............................................................

MBELE YA:
Jina: .......................................................
Wadhifa: ....................................................
Saini ..........................................................
Tarehe ........................................................

Lakiri ya Halmashauri ya Mji Njombe imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia Azimio lililopitishgwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri yam ji Njombe uliuofanyika tarehe 3/5/2023 na kushuhudiwa lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

KURUTHUM A. SADIK,
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Mji Njombe*

ERASTO B. MPETE,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Mji Njombe*

**L.S**

**NAKUBALI**,

Dodoma,
29 Agosti, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB.),
Waziri wa Nchi OR-Tamisemi